# NEW LIFE

# IMANI YA WABATISTI

# NEW LIFE

# IMANI YA WABATISTI

Compiled by D. R. Dolifka

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

© Copyright, 1986
Baptist Publications House
All Rights Reserved



## VI. SITA, WABATISTI NI TOFAUTI KATIKA NJIA AMBAZO TUNATOA NA KUTUMIA PESA

Sisi Wabatisti hutoa pesa kwa sababu tunafuata mafundisho ya Biblia na uongozi wa Roho Mtakatifu. Sisi hutoa sadaka na zaka kwa sababu tunashawishiwa na upendo na mahitaji. Mali ya Wabatisti haihesabiwi kwa ajili ya ushuru au utoaji wa kodi ya makanisa. Twafuata mafundisho ya Biblia katika kuleta zaka na sadaka zetu pale kanisani kulingana na mapato yetu. Kanisa lenyewe ndilo huamua jinsi litakavyogawanya zaka na sadaka katika huduma zao na ushirika wa Wabatisti wengine. Zawadi kutoka kwa makanisa mengi ya Kibatisti hukusanywa pamoja kwa ajili ya huduma za umisheni na huduma ya kuwafadhili watu wenye mahitaji. Wabatisti wanaamini ya kwamba kanisa lazima lijitegemeze lenyewe, lakini mara kwa mara wanasaidiana wenyewe kwa wenyewe.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je. njia sita Wabatisti ni tofauti ni nini?

JIBU: Kwanza, Wabatisti ni tofauti katika historia yetu.
Pili: Wabatisti ni tofauti katika njia ya kutii Biblia.
Tatu, Wabatisti ni tofauti kwa sababu tuko huru, na hali tumejitolea kushirikiana pamoja.
Nne, Wabatisti ni tofauti jinsi jumuiya ya makanisa katika wilaya inavyofanya kazi.
Tano, Wabatisti ni tofauti jinsi ya makanisa yote nchini inavyofanya kazi.
Sita, Wabatisti ni tofauti katika njia ambazo tunatoa na hutumia pesa.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**"Yesu akaja kwao, akasema, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkibatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28:18-20**

Jumuiya ya makanisa yote nchini hufuata mapenzi ya makanisa. Na mapenzi haya ya makanisa hufikiwa katika mkutano wa mwaka ambapo Wabatisti wengi hushiriki. Wao hutayarisha mwongozo na shabaha. Kufuatana na yake waliyosadiki na yanasifa njema ya kikazi. Wafanya kazi wa jumuiya (maofisa, wanakamati, na walioajiriwa na jumuiya) hufuata shabaha na maongozi haya kadiri wanavyoendelea kufanya kazi. Jumuiya ya makanisa yote nchini haitoi maagizo kwa makanisa; bali hushauri katika mambo ya utaratibu wa ushirika na kazi ya Mungu. Jumuiya hutoa njia ya utaratibu kwa ajili ya makanisa ili kuwasiliana na kupanga kazi zao pamoja kadiri wanavyofuata uongozi wake Mungu.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, ni lazima kwa makanisa kufuata mapenzi ya jumuiya?
JIBU: **Hapana, nilazimu kwa jumuiya kufuata mapenzi ya makanisa.**

SWALI: Je, njia tano Wabatisti ni tofauti ni nini?
JIBU: **Kwanza, Wabatisti ni tofauti katika historia yetu.**
**Pili, Wabatisti ni tofauti katika njia ya kutii Biblia.**
**Tatu, Wabatisti ni tofauti kwa sababu tuko huru na hali tumejitolea hushirikiana pamoja.**
**Nne, Wabatisti ni tofauti jinsi jumuiya ya makanisa katika wilaya inavyofanya kazi.**
**Tano, Wabatisti ni tofauti jinsi ya makanisa yote nchini inavyofanya kazi.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++



YALIYOMO


| | Ukurasa |
|---|---|
| 1. Maisha Mapya | 1 |
| 2. Kanisa I | 7 |
| 3. Kanisa II | 12 |
| 4. Ubatizo | 16 |
| 5. Chakula cha Bwana | 21 |
| 6. Mungu I | 25 |
| 7. Mungu II | 29 |
| 8. Yesu Kristo I | 34 |
| 9. Yesu Kristo II | 38 |
| 10. Roho Mtakatifu | 43 |
| 11. Dhambi na Shetani I | 48 |
| 12. Dhambi na Shetani II | 52 |
| 13. Hukumu I | 56 |
| 14. Hukumu II | 60 |
| 15. Makao ya Milele | 64 |
| 16. Wabatisti ni Tofauti I | 69 |
| 17. Wabatisti ni Tofauti II | 76 |

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, jumuiya hutumika kanisa kwa juhudi za pamoja, kwa mambo gani?

JIBU: **Jumuiya hutumika kanisa kwa juhudi za pamoja kwa mambo yale kanisa moja haliwezi kutimiza peke yake.**

SWALI: Je, kazi ya wajumbe ni kufanya nini katika mkutano ya jumuiya?

JIBU: **Kazi ya wajumbe ni kutoa ripoti katika makanisa wanayotoka na kujaribu kuongoza washiriki kujitolea kwa ushirika katika utaratibu wa kazi.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Kiasi cha utaratibu wa kazi unategemea jinsi makanisa yanavyotoa misaada kwa hiari yao wenyewe. Kwa sababu ya uhusiano wa kila mara na makanisa, jumuiya ya makanisa katika wilaya inaweza kujishughulisha haraka katika mahitaji kanisani kuliko jumuiya ya makanisa yote nchini.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, njia nne Wabatisti ni tofauti ni nini?

JIBU: **Kwanza, Wabatisti ni tofauti katika historia yetu.**
**Pili, Wabatisti ni tofauti katika njia ya kutii Biblia.**
**Tatu, Wabatisti ni tofauti kwa sababu tuko huru, na hali tumejitolea hushirikiana pamoja.**
**Nne, Wabatisti ni tofauti jinsi jumuiya ya makanisa katika wilaya inavyofanya kazi.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## V. TANO, WABATISTI NI TOFAUTI JINSI YA MAKANISA YOTE NCHINI INAVYOFANYA KAZI.

Jumuiya ya makanisa yote nchini huwepo kuwezesha makanisa yote nchini katika kutimiza mpango wa Mungu; husaidia makanisa kutii Agizo Kuu la Yesu (Mathayo 28:18-20). Pia hutoa mipango ya kujitolea katika ushirika wa kutuma wamisheni.

# WABATISTI NI TOFAUTI

# 2

MARUDIO:

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, njia tatu Wabatisti ni tofauti ni nini?

JIBU: **Kwanza, Wabatisti ni tofauti katika historia yetu.**
**Pili, Wabatisti ni tofauti katika njia ya kutii Biblia.**
**Tatu, Wabatisti ni tofauti kwa sababu tuko huru, na hali tumejitolea hushirikiana pamoja.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## IV. NNE, WABATISTI NI TOFAUTI JINSI JUMUIYA YA MAKANISA KATIKA WILAYA INAVYOFANYA KAZI.

Ushirika wa makanisa katika wilaya husaidia kanisa kuwa katika hali ambayo Mungu anaitaka. Jumuiya hutumika kanisa kwa juhudi za pamoja, kwa mambo yake kanisa moja haliwezi kutimiza peke yake. Jumuiya hutoa ushirika na kutia moyo katika makanisa, wakati wajumbe wanapokutana pamoja kusikiliza ripoti na mambo mbali mbali kutoka makanisa. Wajumbe hawa hutoa ripoti katika makanisa wanayotoka, na kujaribu kuongoza washiriki kujitolea kwa ushirika katika utaratibu wa kazi.



# MAISHA MAPYA

## DIBAJI

Kwa mistari iliyotangulia tuliongea juu ya Mungu na binadamu. Mwanadamu kwa hiari yake amefanya dhambi. Anahitaji maisha mapya. Kwa kifo chake cha upatanisho na ufufuo wake, Kristo alifungua njia ya maisha mapya kwa watu wote. Lakini hiyo haithibitishi kuwa wote wataokolewa. Kuna masharti ya kufuatwa kabla ya mtu kuokolewa.

## MAISHA MAPYA

Kuna sehemu mbili katika maisha mapya. Ile sehemu takatifu, na sehemu ya kibinadamu; sehemu ya Mungu na sehemu ya mwanadamu. Sehemu takatifu ni kuzaliwa kupya ambako ni tendo la Mungu. Hapa tunajaribu kufikiria sehemu ya mwanadamu katika maisha mapya. Upande wa mwanadamu wokovu ni kugeuka. Wakati mtu anapogeuka, maisha yake yote hubadilika. Kuna hatua nne za kugeuka:

1. Hatua ya kwanza: **Ona dhambi zetu.**
2. Hatua ya pili: **Tubu dhambi zetu.**
3. Hatua ya tatu: **Weka imani yetu katika Yesu Kristo.**
4. Hatua ya nne: **Tutoke dhambini.**

## I. ONA DHAMBI ZETU

Mtu ni lazima afanye nini ili apate maisha mapya? Kwanza ni lazima aione dhambi yake yeye mwenyewe. Biblia hutuelezea kwamba kila mtu amefanya dhambi.

"Kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."

Warumi 3:23

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, mtu anaweza kutubu dhambi zake ikiwa hajui ana dhambi?

JIBU: LA, MTU HAWEZI KUTUBU DHAMBI ZAKE IKIWA HAJUI ANA DHAMBI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Katika kitabu cha Luka twasoma juu ya watu wawili waliokwenda kanisani kusali.

**"Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali, mmoja Farisayo, wa pili mtoza ushuru. Yule Farisayo akasimama akiomba hivi moyoni mwake; Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi, wadhalimu, wazinzi, wala kama huyu mtoza ushuru. Mimi nafunga mara mbili juma; hutoa zaka katika mapato yangu zote. Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipiga-piga kifua akisema, Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi...."**

**Luka 18:10-13**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Farisayo aliiona dhambi yake?
JIBU: LA.

SWALI: Je, mtoza ushuru aliiona dhambi yake?
JIBU: NDIYO.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Farisayo alifikiri kwamba alikuwa mtu mwema. Alifikiri kwamba hakuwa kama watu wengine. Mtoza ushuru alipiga kifua chake. Alimwomba Mungu kumrehemia. Alijiita mwenye dhambi,





++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, njia tatu Wabatisti ni tofauti ni nini?


JIBU: **Kwanza, Wabatisti ni tofauti katika historia yetu.**

**Pili, Wabatisti ni tofauti katika njia ya kutii Biblia.**

**Tatu, Wabatisti ni tofauti kwa sababu tuko huru, na hali tumejitolea hushirikiana pamoja.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Lakini Wabatisti ni tofauti! Kwa miaka mamia mingi Wabatisti wameishi na kufanya kazi kwa uhuru. Biblia ikiwa ndiyo mwongozo wenye mamlaka, makanisa yamejitolea kwa hiari kufanya kazi katika ufalme wa Kristo ushirika.








++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**SWALI:** Je, hatua ya kwanza ambacho ni lazima tufanye ili tupate maisha mapya ni nini?

**JIBU:** NI LAZIMA KUONA DHAMBI ZETU

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## II. HATUA YA PILI YA MAISHA MAPYA: TUBU DHAMBI ZETU.

Baada ya sisi kuona dhambi zetu, ni lazima kutubu dhambi zetu. Hii ndiyo hatua ya pili kuhakikisha maisha mapya.

Tukitubu dhambi zetu, Mungu atatusamehe. Mungu huondoa dhambi zetu. Mungu hufanya hivi kwa maana Yesu Kristo alilipa gharama ya dhambi zetu. Kifo cha Yesu Kristo msalabani ni dhabihu kwa dhambi zetu. Tukitubu dhambi zetu, Mungu huziosha katika damu ya Yesu Kristo. Mungu husamehe dhambi na kuzisahau. Yeremia alitupatia maneno ya Mungu mwenyewe juu ya hii.

> "...nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena." Yeremia 31:34

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**SWALI:** Tuanapotubu dhambi zetu, tunazifunua mbele ya nani?

**JIBU:** YESU KRISTO.

**SWALI:** Je, hatua mbili za kwanza ni zipi?

**JIBU:** ONA DHAMBI ZETU NA TUBU DHAMBI ZETU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## III. HATUA YA TATU YA MAISHA MAPYA: WEKA IMANI YETU KATIKA YESU.

Hatuwezi kujiokoa. Mungu ndiye hufanya hii. Ni lazima tuamini yake Mungu alisema juu ya Yesu. Tuweka imani yetu katika Yesu Kristo. Hiyo ndiyo hatua ya tatu ya maisha mapya.

"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako, ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka."
Warumi 10:9

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
**SWALI:** Tukiweka imani yetu katika Yesu Kristo, tutafanyiwa nini?
**JIBU:** TUTAOKOKA, TUTAPATA MAISHA MAPYA.
++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Kuweka imani yetu katika Yesu Kristo maana yake ni nini? Ni kama sisi mzima kujipumzisha katika Yesu Kristo. Ikiwa tunaketi kitini, hatuogopi kwamba tutaanguka. Tunapumzisha mwili wetu wote kitini humo. Ni lazima tujipumzishe katika Yesu Kristo vivyo hivyo. Tumefanya kile ambacho alituambia. Tumeiona dhambi yetu. Tumetubu dhambi yetu. Sasa tuweke imani yetu kwake na atatuokoa.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
**SWALI:** Katika hatua ya tatu ya maisha mapya, twaweka imani yetu katika nani?
**JIBU:** TWAWEKA IMANI YETU KATIKA YESU KRISTO.
++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++


Hatua ya tatu ni: Weka imani yetu katika Yesu Kristo. Umpokee moyoni mwako kwa imani. Hii hukufanya mwana wa Mungu. Mungu asema hivyo:

"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu."
Yohana 1:12





Mpango wa utawala wa juu hutumiwa na kanisa la Kikatoliki ambapo Baba Mtakatifu, Askofu, na wengine hutawala kanisa. Pia, mpango wa utawala wa juu, hutumiwa na madhehebu mengine, mahali ambapo kanisa liko chini ya utawala wa Askofu au kamati kuu.



## II. WABATISTI NI TOFAUTI KATIKA NJIA YA KUTII BIBLIA.

Sisi Wabatisti tunajulikana kama "watu wa Biblia." Biblia ni ufunuo wa Mungu kwa wanadamu. Hiyo peke yake ndiyo kanuni yetu katika maisha ya wanadamu. Wabatisti kila mahali katika ulimwengu tunakubali Biblia kuwa msingi wa imani na matendo yetu. Kristo, aliye kiini cha mafundisho ya Biblia, ndiye Mwokozi, Bwana, Mwalimu, na Mfano wetu. Msingi wa matendo ya Wabatisti ni upendo kwa Mungu, Mwanawe Yetu Kristo, heshima kwa kanisa na Neno la Mungu.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, msingi wa matendo ya Wabatisti ni nini?

JIBU: **Msingi wa matendo ya Wabatisti ni upendo kwa Mungu, Mwanawe Yesu Kristo, heshima kwa kanisa na Neno la Mungu.**

SWALI: Je, njia mbili Wabatisti ni tofauti ni nini?

Jibu: **Kwanza, Wabatisti ni tofauti katika historia yetu.**
**Pili, Wabatisti ni tofauti katika njia ya kutii Biblia.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## III. TATU, WABATISTI NI TOFAUTI KWA SABABU TUKO HURU, NA HALI TUMEJITOLEA KUSHIRIKIANA PAMOJA.

Makanisa ya Kibatisti katika kila sehemu ya ulimwengu yanafanya kazi pamoja kwa moyo wa ushirika. "Uhuru na Ushirika" ndio mwongozo wa Wabatisti.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, mwongozo wa Wabatisti ni nini?

JIBU: **Mwongozo wa Wabatisti ni "UHURU NA USHIRIKA."**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Mpango wa utawala wa juu hutumiwa na kanisa la Kikatoliki ambapo





++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Tukiweka imani yetu katika Yesu Kristo, je, tunaweza kuwa na hakika kwamba tumeokolewa?

JIBU: **NDIYO.**

SWALI: Je, hatua tatu za kwanza ya maisha mapya ni nini?

JIBU:
1. **ONA DHAMBI ZETU.**
2. **TUBU DHAMBI ZETU.**
3. **WEKA IMANI YETU KATIKA YESU KRISTO.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## IV. HATUA NNE ZA MAISHA MAPYA: TUTOKE DHAMBINI.

Tuwekapo imani yetu katika Kristo, yeye husamehe dhambi zetu. Anakufanya safi. Hatutaki kuwa mchafu tena. Tugeuke kutoka dhambini. Nabii Isaya alituambia la kufanya:

> **"Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake."**
> **Isaya 55:7**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Mtu mwovu na afanyeje na njia yake?

JIBU: **NI LAZIMA AACHE NJIA YAKE.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Tuwekapo imani yetu katika Yesu Kristo, yeye hutusamehe dhambi zetu. Tusizirudie tena. Tunapaswa kuziacha njia zetu za zamani. Tunapaswa kukoma kutenda dhambi tulikuwa tukizitenda. Sisi hatuwezi kufanya hivi peke yetu. Lakini Yesu Kristo hutupa uwezo wa kuifanya.

Mtu aliye na hakika na maisha mapya yake haendelei kutenda dhambi za maisha yake ya zamani. Tazama yale Yesu Kristo alimwambia mwanamke aliyekamatwa katika uasherati:

**"Yesu akamwambia, 'Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena."**

**Yohana 8:11**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Yesu alimwambia mwanamke asifanye nini baada ya kusamehe?

JIBU: YESU ALIMWAMBIA ASIFANYE DHAMBI TENA.

SWALI: Hatua ya nne ya kupata maisha mapya ni ipi?

JIBU: TUTOKE DHAMBINI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Watu wengine hufikiri wana nguvu nyingi baada ya Mungu kuwasamehe. Wanafikiri wanaweza kukaribia dhambi bila kutenda. Wanafikiri dhambi haiwezi kuwashinda. Methali ya Kiingereza inasema: "Ukicheza na moto utachomeka." Tunaweza kugeuka kutoka dhambi zetu kwa kweli. Lakini ni lazima tutakaa mbali na mahali tulizitenda.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, hatua nne za maisha mapya ni nini?

JIBU:
1. ONA DHAMBI ZETU
2. TUBU DHAMBI ZETU.
3. WEKA IMANI YETU KATIKA YESU KRISTO.
4. TUTOKE DHAMBINI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





Katika Matendo ya Mitume 15:22 twasoma hivi:

**"...ilionekana vyema na mitume, wazee na kanisa lote..." Matendo 15:22**

Kuna mifano zaidi katika Biblia ambapo washiriki wa kanisa walifikia uamuzi wao wenyewe. Katika historia ya Biblia, waamini walikuwa sawa mbele za Mungu. Walikuwa na umoja na uhuru wa kiroho katika Kristo. Wabatisti wamefuata kanuni hizi za imani kutoka wakati wa Biblia hadi wakati huu.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Katika historia ya Biblia, waamini walikuwa sawa mbele za Mungu?

JIBU: **Ndiyo, walikuwa sawa mbele za Mungu.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Kama Wakristo wale wa kwanza, Wabatisti wa Ulaya na Amerika wanaamini ya kwamba kila kanisa lina uhuru wa kukata shauri juu ya mapenzi ya Mungu kwa ajili ya kanisa lao. Kila mahali katika ulimwengu, na hasa hapa Afrika, makanisa ya Kibatisti yanajiongoza yenyewe. Kila kanisa linafikia uamuzi wao, kwa mfano, kumwita mchungaji fulani kuhudumia kanisa lao. Kila kanisa ni shirika la watu waliozaliwa mara ya pili, ambao wana shauku ya kushuhudia watu wa kijiji chao au eneo lao na ulimwengu wote kwa jumla.

Leo sisi Wabatisti tunaendelea kukataa utawala wa kikundi fulani. Tunakumbuka urithi wetu wa kibiblia kuhusu uhuru kama jambo la maana sana.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kwanza Wabatisti ni tofauti kwa njia gani?

JIBU: **Kwanza, Wabatisti ni tofauti katika historia yetu.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, mipango na desturi za madhehebu mengine inaweza kufanya kazi kama zikitumika katika makanisa ya Kibatisti?

JIBU: **Hapana, mipango na desturi za madhehebu mengine haiwezi kufanya kazi kama zikitumika katika makanisa ya Kibatisti.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## I. KWANZA, WABATISTI NI TOFAUTI KATIKA HISTORIA YETU.

Kama Wabatisti twajua ya kwamba ni lazima tufuate Biblia. Twajifunza kutoka katika Agano Jipya ya kwamba kila kanisa lilikuwa huru kufanya mapenzi ya Mungu. Washiriki wa kanisa ni sehemu ya jamii ya Mungu.

**"Maana Mungu hambagui mtu ye yote."**
**Warumi 2:11.**

Wabatisti tuna asili yetu ya kihistoria katika Agano Jipya. Kwa mfano, Matendo ya Mitume mlango wa sita unaeleza ya kwamba washiriki wa kanisa waliwachagua wanaume waliostahili kufanya kazi ya Mungu. Katika Matendo ya Mitume mlango wa 13 washiriki wa kanisa waliwatuma wamisheni.

**"Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia. Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao."**
**Matendo 13:2-3**





# KANISA

# 1

## DIBAJI

Wakati mjenzi anapojenga nyumba, ni lazima afuate mchoro uliochorwa Mungu ametupatia mpango wake wa kanisa katika Agano Jipya. Ni lazima tufuate mipango yake kwa usawa ikiwa tunataka kujenga makanisa yatakayompendezwa Mungu.

Hatuzungumzi juu ya nyumba. Kanisa ni watu. Sio nyumba. Yesu anawatumia watu walio Wakristo kujenga kanisa lake. Wakristo ni kama mawe Yesu anavyotumia. Yesu ni msingi wa kanisa. Wakristo ni mawe ya majengo. Na pia Yesu ni kichwa cha kanisa.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kanisa ni nyumba?

JIBU: **HAPANA. KANISA NI WATU WA KRISTO.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Neno "kanisa" limetajwa mara 114 katika Agano Jipya. Karibu kila mahali neno hili hutaja kikundi cha Wakristo wanaoishi na kuabudu katika mahali fulani. Kuna mara chache neno hili kutajwa kuwa waaminio wote waliozaliwa mara ya pili. Wakati neno "kanisa" hutajwa namna hii tunalifikiria kama ufalme wa Mungu.

Kama tutakavyojifunza juu ya kanisa tutafahamu kwamba kanisa la mahali pamoja linaloonekana na linalojiongoza.

Kanisa linaonekana kwamba laweza kuelezwa kama kikundi cha waaminio waliobatizwa, wanaojiunga kwa hiari na kuunganishwa na ahadi iliyoundwa kufuatisha mfano wa Agano Jipya. Wanajaribu kuishi kwa kumtii Kristo, aliye mkuu wa kanisa.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kanisa ni nini?

JIBU: KANISA NI KAMA KIKUNDI CHA WAAMINIO WALIOBATIZWA.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

USHIRIKA WA KANISA NI NINI?

Kuna mambo yalioyotajwa katika Agano Jipya ambayo huhitajika kwa mtu akitaka kuwa mwanachama wa kanisa.

1. Ni lazima wazaliwe mara ya pili. Washiriki wa kanisa ni lazima wawe wamekubali Kristo kama Mwokozi. Washiriki wote wa kanisa hukiri, kuwa wamezaliwa mara ya pili na waliopita kutoka mautini kwa maisha katika Yesu Kristo. Watu wa kanisa huwa na tofauti na watu wengine kwa sababu wana matumaini ya maisha ya milele. Ushirika ni kwa hiari.....yaani mtu kuchagua kumpokea na kumfuata Yesu.

"Bwana akalizidisha kanisa kila siku
kwa wale waliokuwa wakiokolewa."
Matendo 2:47

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, mambo la kwanza ambalo ni lazima ufanye ukitaka kuwa mwanachama wa kanisa ni nini?

JIBU: NI LAZIMA WAZALIWE MARA YA PILI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





# WABATISTI NI TOFAUTI

# 1

## DIBAJI

HARAKA Bwana! Ninahitaji kifaa fulani kwa ajili ya motokaa yangu," akasema mzee Juma. Naye makanika akasema, "Vema, ebu na tutumie kifaa hiki ambacho kilitoka kwa baisikeli na tukiweke katika motokaa yako."

Kusema kweli, vifaa vya baisikeli havitaweza kufanya kazi katika motokaa. Vivyo hivyo, mipango na desturi za madhehebu mengine haziwezi kufanya kazi kama zikitumika katika makanisa ya Kibatisti.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, vifaa vya baisikeli vitaweza kufanya kazi katika motokaa?

JIBU: Hapana, vifaa vya baisikeli havitaweza kufanya kazi katika motokaa.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Wabatisti ni tofauti! Kanuni zinazotolewa hapa na pale kutoka madhehebu mengine hazitakuwa za manufaa kwa Wabatisti. Makanisa ya Kibatisti, jumuiya ya makanisa katika wilaya, na jumuiya ya makanisa yote nchini zinahitaji kufanya kazi Kibatisti kamili kwa kila tendo.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, jehanum ni mahali gani?

JIBU: 1. JEHANUM NI MAHALI PA HAKIKA.

2. JEHANUM NI MAHALI AMBAPO PASIPOEPUKIKA.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

3. <u>Jehanum ni mahali pa wale ambao wamekataa huruma ya Mungu katika Yesu Kristo.</u> Mungu hataki mtu awaye yote aende jehanum.

"Maana hapendi mtu yeyote apotee,
bali wote wafikilie toba."
II Petro 3:9

Kwa sababu ya upendo wake kwetu, Mungu alitengeneza njia ya wokovu kwa kumtuma Yesu afe badala yetu. Ikiwa mtu hupenda njia za dhambi hata hukataa kutubu na kumwamini Yesu, basi ni lazima alipiwe mshahara wa dhambi zake.

"Amwaminiye hahukumiwi, asiye-
amini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu
hakuliamini jina la Mwana pekee wa
Mungu. Na hili ndiyo hukumu; ya kuwa
nuru imekuja ulimwenguni, na watu waka-
penda giza kuliko nuru, kwa maana matendo
yao yalikuwa maovu."
Yohana 3:18-19

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, jehanum ni mahali gani?

JIBU: 1. JEHANUM NI MAHALI PA HAKIKA.

2. JEHANAM NI MAHALI AMBAPO PASIOPOEPUKIKA.

3. JEHANAM NI MAHALI PA WALE AMBAO WAMEKATAA HURUMA YA MUNGU KATIKA YESU KRISTO.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





2. Walio washiriki wa kanisa ni lazima wabatizwe. Hakuna mahali popote katika Agano Jipya ambapo washiriki wa kanisa hawakuwa wamebatiza.

"Wao waliolipokea neno lake
wakabatizwa."
Matendo 2:41

Kitendo cha ubatizo ni kitendo cha kwanza kwa kumtii Kristo. Wakati huu mtu huwa amepita kutoka kifoni mpaka maishani ni cha hiari. Ubatizo ni kama kuandikiana kwa maagano na Mungu kuishi na yeye maisha ya uaminifu na usafi.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, mambo mawili ya kwanza ambayo ni lazima kufanya ukitaka kuwa mwanachama wa kanisa ni nini?

JIBU: NI LAZIMA WAZALIWE MARA YA PILI NA NI LAZIMA WABATIZWE.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Je, ubatizo una uwezo wa kumsaidia mtu kuokolewa? Hapana. Ubatizo hauwezi kumsaidia mtu kuokolewa hata kidogo. Imani tu, inaleta wokovu.

3. Walio washiriki wa kanisa ni lazima wawe waaminifu.
Yesu alisema:

"Mkinipenda, mtazishika amri zangu."
Yohana 14:15

Washiriki wa kanisa hawapaswi tu kujifunza vile Yesu hufundisha lakini hutaka kuzitii amri zake.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**SWALI:** Je, mambo matatu ambayo ni lazima kufanya ukitaka kuwa mwanachama wa kanisa ni nini?

**JIBU:** **NI LAZIMA WAZALIWE MARA YA PILI, WABATIZWE, NA WAWE WAAMINIFU.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**MFANO WA AGANO JIPYA KWA KULIONGOZA KANISA NI WA AINA GANI?**

Kuna mambo mawili makubwa:

**(1)** Kanisa la Agano Jipya hutawaliwa na washiriki wote.

A. KANISA LA AGANO JIPYA HUWA NA WASHIRIKI WALIOJIUNGA KWA HIARI. Kanisa huundwa na watu ambao huingia ushirika wake kwa sababu hupenda kuingia. Hakuna mtu ye yote aliye mshiriki wa kanisa kwa kuzaliwa. Hakuna mtu anayestahili kupelekwa kanisani bila hiari yake.

B. KILA MSHIRIKI WA KANISA LA AGANO JIPYA ANA HAKI SAWASAWA. Kila mshiriki ana uwezo sawasawa pia. Wazee na vijana, mtajiri na maskini, wenye elimu na wale wasio na elimu wako katika haki sawa. Hakuna mtu aliye na uwezo kuiondoa katiba ya kanisa.

C. KICHWA CHA KANISA LA AGANO JIPYA NI BWANA YESU KRISTO. Tumekwisha kuona mapema katika somo hili kuwa Kristo ni kichwa cha kanisa. Hata hivyo, ni Kristo katika Roho Mtakatifu ambaye anaongoza kila Mkristo na kuuongoza mwili wa kanisa.

D. KANISA LA AGANO JIPYA HUJITAWALA LENYEWE. Kanisa ni kikundi chenye kujitawala. Hakuna mtu binafsi wala kikundi juu ya kanisa kilicho na uwezo juu yake. Kila kanisa chini ya uongozi wa Mungu huendesha mambo yake.





++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**SWALI:** Je, mbinguni kutakuwa mahali pa uhuru kutokana na uovu wa asili kama nini?

**JIBU:** **MBINGUNI KUTAKUWA MAHALI PA UHURU KUTOKANA NA UOVU WA ASILI KAMA HUZUNI, MAGONJWA NA KIFO.**

**SWALI:** Je, mbinguni itakuwa kuondolewa kabisa kutoka wapi?

**JIBU:** **MBINGUNI ITAKUWA KUONDOLEWA KABISA KUTOKA DHAMBINI.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

JEHANUM

1. <u>Jehanum ni mahali pa hakika.</u> Kuna watu hukataa kuwa mahali pa uchungu wa milele tunaoufahamu kama jehanum. Mtu anaweza kukana kuwa hakuna jua, lakini lingali lipo tu. Biblia hufundisha wazi kuwa jehanum ni mahali pa kweli na ya kwamba Yesu alikufa ili tuokolewe nayo.

> **"Watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake."**
> **II Wathesalonike 1:9**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**SWALI:** Je, jehanum ni mahali gani?

**JIBU:** **JEHANUM NI MAHALI PA HAKIKA.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

2. <u>Jehanum ni mahali ambapo pasiopoepukika.</u> Mungu huwapatia watu wote huruma yake kwa njia ya Yesu Kristo. Lakini wakati ambapo mtu huishi halafu kufa akiwa amekataa huruma hii ya Mungu basi, hakuna tumaini kwake. Hakuna nafasi ya pili au kukimbia kutoka jehanum.

> **"Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze; wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu."**
> Luka 16:26

3. <u>Mbinguni itakuwa maisha ya ushirika pamoja na Mungu kwa njia ya Kristo.</u> Ushirika pamoja na Mungu ndiyo furaha yake kuu kwa maisha hayo. Ni hiyo ambayo huleta furaha tumaini na uwezo. Ni ushirika mkamilifu pamoja na Bwana ambao Mkristo hutaka kupata katika maisha yajayo. Paulo alisema ni bora sana kwenda kwa njia ya kifo na kuishi pamoja na Bwana.

**"Ninasongwa katikati ya mambo mawili; ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo; maana ni vizuri zaidi sana." Wafilipi 1:23**

Hili ni elezo la hamu ya tazamio la kurudi mara ya pili ambayo huonekana katika Agano Jipya.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, mbinguni itakuwa maisha ya ushirika pamoja na nani?
JIBU: **MBINGUNI ITAKUWA MAISHA YA USHIRIKA PAMOJA NA MUNGU KWA NJIA YA KRISTO.**
SWALI: Je, mbinguni ni wapi?
JIBU: **MBINGUNI NI HALI AMBAYO WAKRISTO WANAJIKUTA BAADA YA KIFO WASHIRIKIANA NA MUNGU.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

4. <u>Mbinguni kutakuwa mahali na uhuru kutokana na uovu wa asili, kama huzuni, magonjwa na kifo.</u>

**"Naye atafuta kila chozi katika macho yao. Ufunuo 21:4**

**"Huzuni na kuugua zitakimbia." Isaya 51:11**

Kutakuwa ushindi juu ya mambo mengine maovu.





++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, jambo la kwanza kwa kuliongoza kanisa la Agano Jipya ni nini?
JIBU: **KANISA LA AGANO JIPYA HUTAWALIWA NA WASHIRIKI WOTE.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

(2) Kanisa la Agano Jipya ni kikundi huru.

A. Lina uhuru kuhusu uhusiano wake na makanisa mengine. Hakuna kanisa lililo na mvuto wala nguvu, lililokubaliwa kuwa juu ya kanisa lingine, iwapo lingalikuwa ndogo kiasi gani.

B. Lina uhuru kwa uhusiano wake na serikali. Taifa haitajiingiza kutawala kanisa au kikundi kingine cha dini. Kanisa au vyama vya dini haistahili kutawala taifa.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, mambo mawili makubwa yalioyoiongoza kanisa la Agano Jipya ni nini?
JIBU: **1. KANISA LA AGANO JIPYA HUTAWALIWA NA WASHIRIKI WOTE.**
**2. KANISA LA AGANO JIPYA NI KIKUNDI KILICHO HURU.**
SWALI: Je, kanisa ni nini?
JIBU: **KANISA NI KAMA KIKUNDI CHA WAAMINIO WALIOBATIZWA.**
SWALI: Je, mambo matatu ambayo ni lazima ufanye ukitaka kuwa mwanachama wa kanisa ni nini?
JIBU: **(1) NI LAZIMA WAZALIWE MARA YA PILI.**
**(2) NI LAZIMA WABATIZWE.**
**(3) NI LAZIMA WAWE WAAMINIFU.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

# KANISA
# 2

MARUDIO:

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kanisa ni nini?
JIBU: KANISA NI KAMA KIKUNDI CHA WAAMINIO WALIOBATIZWA.

SWALI: Je, mambo matatu ambayo ni lazima ufanye ukitaka kuwa mwanachama wa kanisa ni nini?
JIBU: (1) NI LAZIMA WAZALIWE MARA YA PILI.
(2) NI LAZIMA WABATIZWE.
(3) NI LAZIMA WAWE WAAMINIFU.

SWALI: Je, mambo mawili makubwa yalioyoiongoza kanisa la Agano Jipya ni nini?
JIBU: 1. KANISA LA AGANO JIPYA HUTAWALIWA NA WASHIRIKI WOTE.
2. KANISA LA AGANO JIPYA NI KIKUNDI KILICHO HURU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





"Lakini, kama ilivyo ahadi yake, tunatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake."
II Petro 3:13

Bila shaka mbinguni itakuwa mahali pia itakuwa hali ya kuishi.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, maana ya mbinguni ni nini?
JIBU: MAANA YA MBINGUNI NI KUWA PAMOJA NA MUNGU KWA MILELE.
SWALI: Je, mbinguni ni wapi?
JIBU: MBINGUNI NI HALI AMBAYO WAKRISTO WANAJIKUTA BAADA YA KIFO WAKISHIRIKIANA NA MUNGU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

2. **Mbinguni itakuwa kutolewa kutoka dhambi.** Kuwa kama Kristo itakuwa mbinguni.

"Twajua ya kwamba atakapodhihirishwa, tutafanana naye." I Yohana 3:2

Tufanywa kama Kristo kwa tabia ndilo jambo ambalo Mungu aliyekuwa nalo katika mawazo yake katika milele. Ni mpango wake tugeuzwe kwa mfano wa Mwanawe.

"Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi." Warumi 8:29

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, mbinguni itakuwa kuondolewa kabisa kutoka wapi?
JIBU: MBINGUNI ITAKUWA KUONDOLEWA KABISA KUTOKA DHAMBINI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

# MAKAO YA MILELE

## DIBAJI

Katika masomo yetu yaliyotangulia tuliona kuwa Biblia hufundisha kuwa kutakuwa na ufufuo wa wote wenye haki na wasio haki. Tumejifunza pia kuwa hukumu ni ya lazima. Baada ya hukumu, kuna mahali tu pa kuishi, mbinguni au jehanum. Kila mtu ataishi milele pengine mbinguni au jehanum. Kwa hiyo, ebu tuone neno la Mungu hufundisha kuhusu mahali hapo pawili.

## MBINGUNI

Maana ya mbinguni ni kuwa pamoja na Mungu kwa milele. Hakuna mtengano tena. Kila Mkristo atakuwa pamoja na Mungu kwa sababu amewahi kuchagua kuwa naye. Tuna ufahamu wa kubarikiwa kukombolewa katika ulimwengu huu. Lakini tunaingia ukamilifu wa maisha hayo ya kubarikiwa katika kifo.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, maana ya mbinguni ni nini?
JIBU: MAANA YA MBINGUNI NI KUWA PAMOJA NA MUNGU KWA MILELE.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

1. Mbinguni ni wapo? Kwanza mbinguni si mahali lakini hali ambayo Wakristo wanajikuta baada ya kifo wakishirikiana na Mungu. Kutakuwa na mbingu mpya na nchi mpya kwa wanadamu wapya ya kuishi.





## VIONGOZI WA KANISA NI NANI?

1. **Mchungaji.** Neno "mchungaji", "mzee", na "askofu" yametumiwa yakibadilishwabadilishwa katika Agano Jipya. Katika Matendo 20:27 Paulo aliwaita wazee wa kanisa la Efeso. Katika Matendo 20:28 aliwaambia Roho Mtakatifu aliwafanya waangalizi (Maaskofu) na ya kwamba watatunza (mchungaji) kanisa. Pengine swali litatukia, Ni nani anayestahili kuwa mchungaji wa kanisa? Twaone ustahilifu uliotolewa na Mungu kwa mchungaji katika I Timotheo 3:1-7 na Tito 1:7-8:

> "Ni neno la kuaminiwa; mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema. Basi imepasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mwenye kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu, (yaani mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje kanisa la Mungu?) Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi. Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi."
>
> Timotheo 3:1-7

> "Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu; asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake, asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi wala mgomvi, asiwe mpenda mapato ya aibu; bali awe mkaribishaji, mpenda mwema, mwenye kiasi, mwenye haki, matakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake."
>
> Tito 1:7-8

Mchungaji angekuwa mtu ambaye angeitwa moyoni mwake na Mungu kwa kushika madaraka ya kutunza kanisa.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kiongozi mmoja wa kanisa ni nani?
JIBU: KIONGOZI MMOJA WA KANISA NI MCHUNGAJI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Kwa nini tunaweka viongozi wa kanisa ikiwa tunajua kwamba kiongozi wake ni Yesu Kristo? Tutasoma Waefeso 4:11-12:

> "Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe."
> Waefeso 4:11-12

Yesu alitoa watu kuwa wachungaji kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeka hata mwili wa Kristo ujengwe. Wachungaji ni vyomba vya Kristo. Wachungaji ni watumishi wa Kristo na kanisa.

2. Mashemasi. Makanisa ya Agano Jipya pia yalikuwa na mashemasi. Ustahilifu wa shemasi umeelezwa katika I Timotheo 3:8-13:

> "Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana, si watu wanaotamani fedha ya aibu; wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye





WALE WATAKAOOKOLEWA KWA NJIA GANI?

Hakuna mtu atakayeokolewa kwa ajili ya wema wake lakini kwa sababu ametubu, amempokea Yesu kuwa Mwokozi wake, na kusimama mbele ya Mungu katika haki ambayo Yesu aliyekufia ili ampe.

> "Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.
> Yohana 3:18

> "Yeye asiyeijua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye."
> II Wakorintho 5:21

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, wale watakaookolewa wataokolewa kwa njia gani?
JIBU: WATAKAOOKOLEWA NI WALE WALIOTUBU DHAMBI NA KUMPOKEA YESU KUWA MWOKOZI WAKE.
SWALI: Je, sababu tatu za kuwepo hukumu ni nini?
JIBU:
1. KUMWONYESHA KILA MTU HALI YAKE YA MAISHA YAKE YOTE.
2. KUMPATIA MTU MAHALI PA KUKAA KUFUATANA NA MAISHA ALIYOISHA DUNIANI.
3. KUHUKUMU WALIMWENGU WOTE.

SWALI: Je, wale watakaohukumiwa ni watu gani?
JIBU: KILA MTU ATAKUWA KATIKA HUKUMU KWA SABABU YA DHAMBI ZAKE MWENYEWE.
SWALI: Je, wale watakaookolewa wataokolewa kwa njia gani?
JIBU: WATAKAOOKOLEWA NI WALE WALIOTUBU DHAMBI NA KUMPOKEA YESU KUWA MWOKOZI WAKE.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## WALE WATAKAOHUKUMIWA

Kila mtu atakuwa katika hukumu kwa sababu ya dhambi zake mwenyewe.

Atadumu katika hukumu hiyo ya Mungu kwa sababu ya kukataa Yesu Kristo kama Mwokozi wake na Bwana. Wakati mtu anapokataa upendo wa Mungu na huruma katika Kristo, hakuna msaada mwingine kwake. Wale ambao hufa wakiwa wamemkataa Yesu kama Mwokozi wao watalaumiwa katika hukumu.

> "Asiyeamini amekwisha kuhukumiwa - kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu. Na hii ndiyo hukumu; yakuwa nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru, kwa maana matendo yao yalikuwa maovu." Yohana 3:18-19

> "Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto." Ufunuo 20:15

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, wale watakaohukumiwa ni watu gani?

JIBU: KILA MTU ATAKUWA KATIKA HUKUMU KWA SABABU YA DHAMBI ZAKE MWENYEWE.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





> waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. Vivyo hivyo wake zao na wewe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote. Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. Kwa maana watendao vema kazi ya shemasi hujipatia daraja nzuri, na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Yesu Kristo.
>
> I Timotheo 3:8-13

Walitengwa mara ya kwanza katika Matendo ya Mitume mlango wa sita. Ingawa mashemasi ni viongozi wa kiroho wenye heshima hawana uwezo wa kutawala washiriki. Kazi yao ni ya utumishi wa kanisa yaani kumsaidia Mchungaji kufanya kazi ya Mungu.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, viongozi vya kanisa na nani?

JIBU: **VIONGOZI WA KANISA NI MCHUNGAJI NA MASHEMASI.**

SWALI: Je, kanisa ni nini?

JIBU: **KANISA NI KAMA KIKUNDI CHA WAAMINIO WALIOBATIZWA.**

SWALI: Je, mambo matatu ambayo ni lazima ufanye ukitaka kuwa mwanachama wa kanisa ni nini?

JIBU:
1. **NI LAZIMA WAZALIWE MARA YA PILI.**
2. **NI LAZIMA WABATIZWE.**
3. **NI LAZIMA WAWE WAAMINIFU.**

SWALI: Je, mambo mawili makubwa yaliyoliongoza kanisa la Agano Jipya ni nini?

JIBU:
1. **KANISA LA AGANO JIPYA HUTAWALIWA NA WASHIRIKI WOTE.**
2. **KANISA LA AGANO JIPYA NI KIKUNDI KILICHO HURU.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

# UBATIZO

## DIBAJI:

Kanisa lina maagizo mawili. Yanaitwa ubatizo na chakula cha Bwana. Ubatizo ndiyo njia ya kuwa mshiriki wa kanisa. Chakula cha Bwana ni kwa wale walio ndani ya kanisa. Maagizo hayo si mambo yaliyotengenezwa na mtu. Yamepeanwa na Yesu mwenyewe. Yalipeanwa ili aonyeshe vile alivyotufanyia. Utii kamili kwa Kristo hudai amri hizi mbili kufuata mfano na njia inaonyesha kwa mfano na mafundisho ya Bwana wetu Yesu.

## UBATIZO

Neno la Kiyunani, ambalo ni "batidzo" ni neno hilo ambalo kimeingizwa kwa Kiswahili yaani, "ubatizo". Maana halisi ya neno hili ni kutia ndani au kuzamisha chini au kuchovya ndani. Katika maandishi va zamani ya Wayunani neno hili ililikuwa likitumiwa wakati mtu aliposema kuhusu kuchuliwa na maji. Kubatizwa, mtu huzamishwa ndani ya maji. Halafu huinuliwa kutoka majini. Kama Yesu alivyofufuka kutoka kaburini. Yesu ametoa tendo hili la ubatizo kuwa kama mfano kwa mtu kuonyesha amepata maisha mapya. Twaona kuwa kanisa la Agano Jipya lilikuwa likifanya ubatizo kwa kuchovya.





## SABABU NYINGINE YA HUKUMU

Sababu ya hukumu ya mwisho ni kuhukumu walimwengu wote. Mungu aliumba mtu kama taifa si kama watu binafsi. Tangu wakati mtu wa kwanza alipotenda dhambi, jamii yote ya watu wametumbukia na dhambi. Mungu alitoa ukombozi katika Kristo Yesu. Imekazwa hasa katika Agano Jipya kuwa hukumu itakuwa kwa watu wote.

> "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake, na mataifa yote wataku-sanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi.
> Mathayo 25:31-32

> "Lakini wewe je! mbona wamhukumu ndugu yako? au wewe je! mbona wamdharau ndugu yako? Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu."
> Warumi 14:10

Watu wote watakuwa hapo. Mambo yote ya historia ya mwanadamu katika duniani yatamalizika.

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, atakayehukumu watu ni nani?
JIBU: YESU KRISTO NDIYE ATAKAYEHUKUMU WATU WOTE.
SWALI: Je, sababu tatu za kuwepo hukumu ni nini?
JIBU:
1. KUMWONYESHA KILA MTU HALI YAKE YA MAISHA YAKE YOTE.
2. KUMPATIA MTU MAHALI PA KUKAA KUFUATANA NA MAISHA ALIYOISHA DUNIANI.
3. KUHUKUMU WALIMWENGU WOTE.

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

# HUKUMU

# 2

MARUDIO:

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kwa nini kuwa na hukumu?
JIBU: KWA UHURU MTU ANAWEZA KUKUBALI AU KUKATAA MUNGU. KWA YEYE HIVYO TUNAHESABIKA KWA MAISHA YETU.
SWALI: Je, tunafundishwa wapi kuhusu hakika ya hukumu ya Mungu?
JIBU: NENO LA MUNGU LINATUFUNDISHA KUHUSU HAKIKA YA HUKUMU YA MUNGU.
SWALI: Je, atakayehukumu watu ni nani?
JIBU: YESU KRISTO NDIYE ATAKAYEHUKUMU WATU WOTE.
SWALI: Je, sababu mbili za kuwepo hukumu ni nini?
JIBU: SABABU HIZO NI;

1. KUMWONYESHA KILA MTU HALI YAKE YA MAISHA YAKE YOTE.
2. KUMPATIA MTU MAHALI PA KUKAA KUFUATANA NA MAISHA ALIYOISHI DUNIANI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





**"Akaamuru lile gari lisimame, wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi, naye akambatiza. Kisha, walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo."**

**Matendo 8:38-39**

Maneno yaliyotumiwa hapa ni kuonyesha ubatizo wa kuchovya.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, maana halisi ya "batizo" ni nini?
JIBU: MAANA HALISI YA 'BATIZO' NI KUTIA NDANI AU KUZAMISHA CHINI AU KUCHOVYA NDANI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**MWANZO WA UBATIZO NI LINI?**

Agizo la ubatizo lilifanywa mara ya kwanza na Yohana Mbatizaji, aliyekuwa ameamriwa kufanya kazi hiyo:

**Palitokea mtu, ametumiwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yohana.**

**Yohana 1:6**

Yohana alidai kuwa alitumwa kubatiza.

**"Lakini yeye aliyenipeleka kubatiza kwa maji."**
**Yohana 1:33**

Yesu alitoa idhini alikubali ubatizo kwa kujitoa mwenyewe kwa ubatizo, kama vile kuonyeshwa na Mathayo 3:13-17. Amri yake kwa wanafunzi wake alipokuwa akiwaacha ilikuwa:

> **Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu."**
>
> **Mathayo 28:19**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Agizo la ubatizo lilifanywa mara ya kwanza na nani?
JIBU: AGIZO LA UBATIZO ILIFANYWA MARA YA KWANZA NA YOHANA MBATIZAJI.

SWALI: Je, maana halisi ya "batizo" ni nini?
JIBU: MAANA HALISI YA 'BATIZO' NI KUTIA NDANI AU KUZAMISHA CHINI AU KUCHOVYA NDANI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## NI NANI ANAYESTAHILI KUBATIZWA?

Ni mtu aliye na imani ya kuokoka katika Yesu ndiye anayestahili kubatizwa. Ubatizo ni kwa mtu aliyemkiri Kristo kwa wazi mbele ya kanisa.

Mtu ye yote ambaye haelewi maana ya ubatizo hawezi kubatizwa kwa kweli. Hakuna mtu anayeweza kubatizwa kwa niabu ya mwingine, au kuokolewa kwa mwingine. Mtu ambaye hajafikia umri wa kuelewa Injili vizuri ili aokolewe hawezi kubatizwa. Agano Jipya halifundishi ubatizo wa watoto. Ubatizo ni kwa hiari baada ya kumkiri Yesu.





wenzake, na kuonyesha vile matendo yake ameyafanyia maisha ya watu wengine.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, sababu ya kwanza ya hukumu ni nini?
JIBU: SABABU YA KWANZA YA HUKUMU NI KUMWONYESHA KILA MTU HALI YAKE YA MAISHA YAKE YOTE.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

2. Sababu ya hukumu ni kumpatia mtu makao yanayopatana na maisha aliyoyaishi duniani. Maana ya hii si kusema ya kwamba mtu atangojea mpaka wakati wa hukumu ili afahamu kama ameokolewa au amepotea. Anafahamu ikiwa amekwisha kumwamini Yesu kama Mwokozi wake. Pia haina maana kuwa wakati wa hukumu ya mwisho kabla ya kujifurahisha na matunda ya maisha mema au maisha mabaya aliyeishi ulimwenguni. Maana yake ni kuwa katika hukumu ya mwisho atapata ujira wote wa maisha mazuri au mabaya. Kwa hiyo, mtu haingii mahali pa makao yake mpaka hukumu ya Kristo.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, sababu mbili za kuwepo hukumu ni nini?
JIBU: SABABU HIZO NI;
1. KUMWONYESHA KILA MTU HALI YAKE YA MAISHA YAKE YOTE.
2. KUMPATIA MTU MAHALI PA KUKAA KUFUATANA NA MAISHA ALIYOISHI DUNIANI.

SWALI: Je, kwa nini kuwa na hukumu?
JIBU: KWA UHURU MTU ANAWEZA KUKUBALI AU KUKATAA MUNGU. KWA YEYE HIVYO TUNAHESABIKA KWA MAISHA YETU.

SWALI: Je, tunafundishwa wapi kuhusu hakika ya hukumu ya Mungu?
JIBU: NENO LA MUNGU LINATUFUNDISHA KUHUSU HAKIKA YA HUKUMU YA MUNGU.

SWALI: Je, atakayehukumu watu ni nani?
JIBU: YESU KRISTO NDIYE ATAKAYEHUKUMU WATU WOTE.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**"Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu."**
**Matendo 17:31**

Yule anayejionyesha mwenyewe kama Mwokozi ndiye ambaye ni lazima watu wasimama mbele yake ili wahukumiwe. Siku moja Yesu alisimama mbele ya Pilato.

**"Mara kulipokuwa asubuhi wakuu wa makuhani walifanya shauri pamoja na wazee na waandishi na baraza nzima, wakamfunga Yesu, wakamchukua, wakamleta mbele ya Pilato. Pilato akamwuliza, Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi? Akajibu, akamwambia, Wewe wasema. Nao wakuu wa makuhani walikuwa wakimshitaki mambo mengi. Pilato akamwuliza tena akisema, Hujibu neno? Tazama ni mambo mangapi wanayokushitaki! Wala Yesu hakujibu neno tena, hata Pilato akastaajabu."** **Marko 15:1-5**

Siku moja ni lazima Pilato asimame mbele ya Yesu.

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
SWALI: Je, atakayehukumu watu ni nani?
JIBU: YESU KRISTO NDIYE ATAKAYEHUKUMU WATU WOTE.
+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## SABABU YA HUKUMU

Je, sababu ya hukumu ni nini? Twaweza kueleza kwa maneno yafuatayo:

1. Sababu ya hukumu ni kuonyesha vile kila mtu alivyo, kama vile maneno yake na matendo yake yameonyeshwa, kama vile amewatendea





+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
SWALI: Je, nani anayestahili kubatizwa?
JIBU: NI MTU ALIYE NA IMANI YA KUOKOKA KATIKA YESU NDIYE ANAYESTAHILI KUBATIZWA.
+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Tukipokea wokovu kwa kuamini Yesu tu, kwa nini twabatizwa? Tutasoma Mathayo 28:19 tena:

"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu."

Mathayo 28:19

Inampasa mtu aaminiye kweli kutafuta ubatizo kwa kuwa ameamriwa na Bwana wake kufanya hivyo. Kwa nini sisi Wabatisti hatubatizi watoto wachanga kama wengine? Sisi hufuata Neno la Mungu tu, maana halituambii juu ya ubatizo wa mtoto mchanga hata moja.

## MAANA YA UBATIZO

Ukweli wa aina tatu hukumbushwa na agizo hili la ubatizo. Ubatizo huonyesha kuzikwa na kufufuka kwa Yesu Kristo. Hutangaza ufahamu wa kugeuzwa kwa maisha ya mwamini. Kifo cha mtu wa kale kwa dhambi, na kufufuka tena kwa mtu mpya ndani ya Kristo. Hueleza tuamini lililobarikiwa la utukufu wa ufufuo wa mwili wakati wa kurudi kwa Bwana:

**"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."**

**Warumi 6:3-4**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, maana halisi ya "batizo" ni nini?
JIBU: MAANA HALISI YA 'BATIZO' NI KUTIA NDANI AU KUZAMISHA CHINI AU KUCHOVYA NDANI.

SWALI: Je, maana ya ubatizo ni nini?
JIBU: KUONYESHA KUFA, KUZIKWA, NA KUFUFUKA KWA YESU KRISTO.

SWALI: Je, nani anayestahili kubatizwa?
JIBU: NI MTU ALIYE NA IMANI NA KUOKOKA KATIKA YESU NDIYE ANAYESTAHILI KUBATIZWA.

SWALI: Je, mtu anaweza kuokolewa kwa njia ya ubatizo?
JIBU: LA, MTU HAWEZI KUOKOLEWA KWA NJIA YA UBATIZO. ANAWEZA KUOKOLEWA KWA NJIA YA KUAMINI TU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





**Kwa uhuru mtu anaweza kukubali au kukataa Mungu. Kwa yeye tunahesabika kwa maisha yetu.** Kipawa cha neema ya Mungu kwa mtu mwenye dhambi hakimtengi mtu kutoka mamlaka yake kwa Mungu. Kwa vile Mungu humshughulikia mtu kwa njia ya neema, kwa hakika neema ya Mungu kwa mtu itahesabika katika hukumu.

**"Atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake." Matendo 2:6**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kwa nini kuwa na hukumu?
JIBU: KWA UHURU MTU ANAWEZA KUKUBALI AU KUKATAA MUNGU. KWA YEYE HIVYO TUNAHESABIKA KWA MAISHA YETU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

HAKIKA YA HUKUMU HUFUNDISHWA WAPI?

**Neno la Mungu hutwaambia kwa hakika ya kuwa itakuja siku wakati Mungu atakapohukumu watu wote.**

**"Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu."**

**Matendo 17:31**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, tunafundishwa wapi kuhusu hakika ya hukumu ya Mungu?
JIBU: NENO LA MUNGU LINATUFUNDISHA KUHUSU HAKIKA YA HUKUMU YA MUNGU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

MTU WA KUHUKUMU NI NANI?

**Maandiko hueleza kuwa Kristo atakuwa hakimu.** Jambo hili ni wazi kwa mistari iliyotajwa hapo juu.

# HUKUMU 1

## Dibaji

Watu wengine huamini kuwa na hukumu zaidi ya moja, wakati wengine hufikiri kuwa itakuwa moja tu. Lakini, wote hukubali ukweli wa hukumu. Katika Agano Jipya lina ukweli huu:

"Kwa maana ameweka siku atakayowa-hukumu walimwengu kwa haki."
Matendo 17:31

"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu." Waebrania 9:27

## KWA NINI KUWA NA HUKUMU?

Sababu ya kuwa na hukumu ni kwa sababu mtu ana wajibu kwa Mungu kama Muumba wa ulimwengu na wa watu. Mtu ana wajibu mbele ya Mungu kwa kuwa Mungu huumba na kumweka aishi na kumpa cho chote alicho nacho katika maisha. Huishi dunia ya Mungu pia. Mungu humpa uhai.

"Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu."
Matendo 17:28





# CHAKULA CHA BWANA

## DIBAJI:

Kanisa lina maagizo mawili. Yanaitwa ubatizo na Chakula cha Bwana. Ubatizo ndiyo njia ya kuwa mshiriki wa kanisa. Chakula cha Bwana ni kwa wale walio ndani ya kanisa. Maagizo hayo si mambo yaliyo-tengenezwa na mtu. Yameanzishwa na Yesu mwenyewe. Yalianzishwa ili aonyesha vile alivyotufanyia. Utii kamili kwa Kristo hudai amri hizi mbili kufuata mfano na njia inaonyesha kwa mfano na mafundisho ya Bwana wetu Yesu.

## CHAKULA CHA BWANA

Chakula cha Bwana kulianzishwa na Bwana wetu katika chumba cha juu kabla ya kifo chake msalabani. Kiwe kikifanywa kama ukumbusho wa kifo chake cha upatanisho.

Mkate uliovunjwa alisema:

" Twaeni, mle, huu ndio mwili wangu."

Mathayo 26:26

Na alipowapa kikombe alisema:

**"Nyweni nyote katika hiki, kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi"**

**Mathayo 26:27-28**

Hakuna uwezo wa kuokoa katika mkate na divai peke yake. Ni kwa ukumbusho na mwili uliovunjika na damu uliyomwagika ya mwokozi.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, chakula cha Bwana kina uwezo wa kuokoa katika mkate na divai peke yake?

JIBU: HAKUNA UWEZO WA KUOKOA. NI KWA UKUMBUSHO TU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

NI NANI ANAYESTAHILI KULA CHAKULA CHA BWANA?

Chakula cha Bwana ni agizo la kanisa, liwe likifanywa na kanisa, na kushirikishwa wote waliofuata masharti yaliyowekwa katika Agano Jipya. Chakula hiki si kwa wale wasioamini; si kwa mtoto asiyefikiri ambaye hawezi kuelewa. Si kwa mtu wa ulimwengu anayeweza kula kwa kujifurahisha tu. Si kwa mnafiki ye yote, ilijionyeshe kwa watu. Ni kwa watu ambao dhambi zao alimesamehewa na kifo chake Kristo Yesu. Chakula cha Bwana hudai mtu ajiangalie kwa uaminifu. Tunastahili kujiangalia sisi wenyewe tuone kama tuna dhambi yo yote ndani yetu. Wakati huo wa Chakula cha Bwana kuziweka mbali na kuuliza Mungu msamaha wake.





**Katika mwali wa moto, huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili wa Bwana wetu Yesu, watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake."**

**II Wathesalonike 1:8-9**

Kuharibiwa huku kwa roho kuitwa sawa kama kifo cha pili. Kuna kuzaliwa kwa mwili na kuzaliwa upya kwa kiroho. Kama hivyo, kuna kifo cha kwanza na kifo cha pili -- kifo cha mwili na kifo cha roho. Yote ni malipo ya dhambi. Na kama vile kuzaliwa kwa kiroho hupendeza kuliko kwa mwili, ndivyo kifo cha roho kilicho kibaya kuliko cha kimwili.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, matukio ya dhambi ni nini?

JIBU: MATUKIO YA DHAMBI NI KIFO CHA MWILI NA ROHO.

SWALI: Je, wenye dhambi ni watu gani?

JIBU: WATU WOTE ULIMWENGUNI NI WENYE DHAMBI.

SWALI: Je, matukio ya dhambi ni nini?

JIBU: MATUKIO YA DHAMBI NI KIFO CHA MWILI NA ROHO.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## MATUKIO YA DHAMBI NI NINI?

Neno moja ambalo hueleza matukio ya dhambi ni "kifo". Dhambi ni kuweka mapenzi yetu juu ya mapenzi ya Mungu. Kufikiri mawazo yetu ni bora kuliko sheria ya Mungu ni dhambi. Dhambi ni maasi ya sheria ya Mungu. Sheria isiyochukua hukumu kwa kuihukumu ya kifo. Kwa Adamu na Hawa alisema:

> **"Kwa maana siku mtakapokula matunda ya mti huo mtakufa hakika."**
>
> Mwanzo 2:17

**Kuna kifo aina mbili na vyote viwili ni matukio ya dhambi:**

1. **Kifo cha mwili**

Kifo cha mwili ni sehemu ya hukumu ya dhambi. Kama hakungalikuwa na dhambi hakungalikuwa na kifo cha mwili. Mungu aliwapa Adamu na Hawa vitu vyote na wangaliepuka kifo, kama hawangalitenda dhambi. Aliweka katika dhambi mti wa uzima, ambao wangalikula matunda yake ni kuishi milele. Mungu alikuwa amewapa njia mabaya wangaliepuka kifo. Lakini badala yake walikula matunda ya mti waliokatazwa. Kutoka siku hiyo, mpaka leo, kifo kimetawala ulimwenguni. Wote waliowahi kuishi ulimwenguni wamekufa.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
SWALI: Tukio moja ya dhambi ni nini?
JIBU: TUKIO MOJA YA DHAMBI NI KIFO CHA MWILI.
++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

2. **Kifo cha Roho**

Maana halisi ya kifo siyo kufa tu, bali mtengano pamoja na uharibifu uendao pamoja nao. Maana ya kifo cha mwili nikutenganishwa mwili na roho. Kifo cha mwili humalizikia katika kifo cha milele cha roho, isipokuwa mtu amekwenda kwa Mungu.





++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
SWALI: Je, ni nani anayestahili kula Chakula cha Bwana?
JIBU: CHAKULA CHA BWANA NI KWA WATU AMBAO DHAMBI ZAO ZIMESAMEHEWA Na KIFO CHAKE KRISTO YESU.
++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## CHAKULA CHA BWANA HUTUKUMBUSHA NINI?

Ahadi hii hutukumbusha kifo na kumwagika damu ya Bwana wetu Yesu Kristo. Alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kwa sababu tulihitaji Mwokozi, na kwa kuwa alitaka kuwa Mwokozi huyo.

Katika Agano la Kale, Mungu alitoa ahadi kuweka Agano Jipya kwa watu wote.

> **"Angalia, siku zinakuja,asema Bwana nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda. Si kwa mfano wa agano lile nililoifanya na baba zao, katika siku ile nilipowashika mkono, ili kuwatoa katika nchi ya Misri; ambalo agano langu hilo walilivunja, ingawa nalikuwa mume kwao, asema Bwana. Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba na Israeli, baada ya siku zile, asema Bwana; Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Wala hawatamfundisha kila mtu jirani yake, na kila mtu ndugu yake, wakisema, Mjue Bwana; kwa maana watanijua wote, tangu mtu aliye mdogo miongoni mwao hata aliye mkubwa miongoni mwao, asema Bwana; maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena."**
>
> Yeremia 31:31-34

Kifo cha Yesu kilikuwa Agano lile. Chakula cha Bwana ni ukumbusho na pia ni nafasi kwa waliomwamini kumsifu Mungu kwa njia yake ya wokovu wa maisha ya milele.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Chakula cha Bwana hutukumbusha nini?
JIBU: **CHAKULA CHA BWANA HUTUKUMBUSHA KIFO NA KUMWAGIKA DAMU YA BWANA WETU YESU KRISTO.**
SWALI: Je, ubatizo na Chakula cha Bwana una uwezo wa kuokoka?
JIBU: **HAPANA, NI KWA UKUMBUSHO TU.**
SWALI: Je, ni nani anayestahili kula chakula cha Bwana?
JIBU: **CHAKULA CHA BWANA NI KWA WATU AMBAO DHAMBI ZAO ZIMESAMEHEWA NA KIFO CHAKE KRISTO YESU.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





"Maana hakuna mtu asiyetenda dhambi."
I Wafalme 8:46

"Tukisema ya kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu." I Yohana 1:10

"Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Warumi 3:23

Wote linaunganisha watu wote wa vizazi vyote ambao wamewahi kujulikana na ulimwengu. Ni zaidi ya mpaka ya nchi kavu na bahari na inahusu mwanadamu ye yote anayeishi ulimwenguni siku hizi. Itakuwa hivyo hata siku zijazo mpaka mwisho wake na vizazi vitakavyokuwako.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Wenye dhambi ni watu gani?
JIBU: **WATU WOTE ULIMWENGUNI NI WENYE DHAMBI.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Huu si ushuhuda tu wa Biblia ni katika ufahamu wetu pia. Mtu ye yote mwanamume au mwanamke mwenye haki hajawahi kupatikana. Hakuna mtu isipokuwa Yesu Kristo aliyeishi maisha bila dhambi. Wale ambao wamekua katika maisha ya Kikristo watakubali kwa urahisi kushindwa kwao na kutenda dhambi bila kukusudia. Wote hawatendi dhambi kwa kimo kimoja, wengine wameingia ndani sana kuliko wengine, lakini hakuna hata mmoja ambaye hajatenda dhambi.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Wenye dhambi ni watu gani?
JIBU: **WATU WOTE ULIMWENGUNI NI WENYE DHAMBI.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

# DHAMBI NA SHETANI

# 2

MARUDIO:

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
SWALI: Je, mwisho wa Shetani ni nini?
JIBU: MWISHO WA SHETANI NI KUADHIBIWA MILELE KATIKA JEHANUM.
SWALI: Je, Shetani ni nani?
JIBU: SHETANI NI MKUU WA ROHO WABAYA.
SWALI: Na kazi ya Shetani ni nini?
JIBU: KAZI YA SHETANI NI KUMPINGA MUNGU NA WOTE WANAOMFUATA.
SWALI: Na mwisho wa Shetani ni nini?
JIBU: MWISHO WA SHETANI NI KUADHIBIWA MILELE KATIKA JEHANUM PAMOJA NA WANAOMFUATA.
SWALI: Maana ya dhambi ni nini?
JIBU: DHAMBI NI KUKATAA MAPENZI YA MUNGU ILI MTU AFANYE MAPENZI YAKE MWENYEWE.
++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

DHAMBI KUWAFIKIA WOTE

Katika Agano la Kale na Agano Jipya twasoma ya kwamba watu wote wamefanya dhambi.





# MUNGU

# 1

**DIBAJI**

Katika somo hili tutajifunza mambo fulani kutokana na mambo ambayo tumesoma kuhusu Mungu katika Biblia. Tutajifunza kuhusu jina lake. Tutajifunza Mungu ana tabia ya aina gani. Tutajifunza kuhusu nafsi tatu katika Mungu wetu mmoja.

Biblia haifanyi mkazi wo wote kuthibitisha kuweko kwake Mungu. Imeanza tu kwa maneno haya:

> **"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi."** **Mwanzo 1:1**

Hii ilifanywa katika mwanzo wa wakati, mwanzo wa dunia hii na vitu vyote.

**JINA LA MUNGU**

Wakati tunapotumia neno "Mungu" hakuna shaka lo lote kuhusu maana yake. Tunamfikiria Mungu mmoja mkuu, (kiumbe chenye uwezo zaidi), Muumba wa vitu vyote. Lakini katika mafikira ya watu wa zamani, kulikuwa na miungu wengi.

Mungu alijipatia jina ambalo angalitambulikana nalo, ili ajitofautishe na miungu wengine:

"Mimi ni BWANA, ndilo jina langu."
Isaya 42:8

Jina la Mungu ni la pekee.

Kuna wengi wa wale huitwa miungu kwa majina mengi siku hizi. Jina la kweli la Mungu ni BWANA: "Mimi ni BWANA, ndilo jina langu." Jina hili BWANA kwa lugha ya Kiebrania Yehova huonyesha au hueleza kuweko kwake Mungu lina mawazo ya asiye na mwisho na asiyebadilika.

Jina la Mungu ni Takatifu. Amri ya tatu ya Musa husema.:

"Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana Mungu hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure."
Kutoka 20:7

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, jina la Mungu ni nini?
JIBU: JINA LA MUNGU NI BWANA.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

MUNGU NI WA NAMNA GANI?

Katika Biblia hupata maneno fulani ambayo hutwambia Mungu ni wa namna gani.

1. <u>Mungu ni roho.</u> Maneno haya yalitajwa na Yesu:





MAANA YA DHAMBI NI NINI?

Kutokana na mambo yanayoonekana tunataka tujifunza hasa maana ya dhambi. <u>Dhambi ni kukataa mapenzi ya Mungu ili mtu afanye mapenzi yake mwenyewe.</u> Hivi ndivyo Adamu na Hawa walivyofanya. Walifahamu mapenzi ya Mungu na wakachagua kuikataa ili waweze kufanya mambo walioyataka kuyafanya.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Maana ya dhambi ni nini?
JIBU: DHAMBI NI KUKATAA MAPENZI YA MUNGU ILI MTU AFANYE MAPENZI YAKE MWENYEWE.

SWALI: Je, mwisho wa Shetani ni nini?
JIBU: MWISHO WA SHETANI NI KUADHIBIWA MILELE KATIKA JEHANUM.

SWALI: Je, Shetani ni nani?
JIBU: SHETANI NI MKUU WA ROHO WABAYA.

SWALI: Na kazi ya Shetani ni nini?
JIBU: KAZI YA SHETANI NI KUMPINGA MUNGU NA WOTE WANAOMFUATA.

SWALI: Na mwisho wa Shetani ni nini?
JIBU: MWISHO WA SHETANI NI KUADHIBIWA MILELE KATIKA JEHANUM PAMOJA NA WANAOMFUATA.

SWALI: Maana ya dhambi ni nini?
JIBU: DHAMBI NI KUKATAA MAPENZI YA MUNGU ILI MTU AFANYE MAPENZI YAKE MWENYEWE.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, mwisho wa Shetani ni nini?
JIBU: MWISHO WA SHETANI NI KUADHIBIWA MILELE KATIKA JEHANUM.
SWALI: Je, Shetani ni nani?
JIBU: SHETANI NI MKUU WA ROHO WABAYA.
SWALI: Na kazi ya Shetani ni nini?
JIBU: KAZI YA SHETANI NI KUMPINGA MUNGU NA WOTE WANAOMFUATA.
SWALI: Na mwisho wa Shetani ni nini?
JIBU: MWISHO WA SHETANI NI KUADHIBIWA MILELE KATIKA JEHANUM PAMOJA NA WANAOMFUATA.

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

DHAMBI

Kabla hatujajifunza juu ya mwanzo wa dhambi, tunataka kupata jibu la swali moja.

Kwa nini Mungu mwenye uwezo wote anayechukia dhambi alikubalia dhambi kuingia duniani? Kama Mungu angaliumba mtu ambaye angalimpa upendo mkubwa na wa kweli pamoja na utii, mtu huyo angalikuwa na uwezo wa kuchukia na kutomtii Mungu.

Mungu hakutaki dhambi iwepo ili watu wasiomtii, bali watu, wamchague, na kumtii katika upendo. Wakati mtu alipochagua kutotii, dhambi iliingia ulimwenguni.

Soma kwa makini Mwanzo 2:8 mpaka 3:24. Mistari hii inatuonyesha dhambi ya kwanza, hutusaidia kufahamu mambo mengi kuhusu dhambi.

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, dhambi iliingia ulimwenguni lini?
JIBU: DHAMBI ILIINGIA ULIMWENGUNI WAKATI MTU ALIPOCHAGUA KUTOTII.

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





"Mungu ni Roho."
Yohana 4:24

Mungu si mtu asiye wa kawaida akiwa na mwili na nyama. Ni wa kiroho. Yeve ana uhuru wa kutozuiwa na kitu cho chote kinachozuia na mwili. Watu wengine humdhania Mungu kama mzee sana ambaye anaketi katika kiti chake cha ukuu mbinguni. Ni shida kwa akili zetu kumfahamu Mungu.

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Mungu ni wa namna gani?
JIBU: MUNGU NI ROHO.

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**2. Pia, Mungu ni nuru.** Haya ni maelezo yaliyotolewa na Yohana kwa Mungu.

**"Mungu ni nuru, wala giza lo lote hamna ndani yake." I Yohana 1:5**

Giza ni mfano wa ujinga, mákosa, na dhambi. Nuru ni mfano wa busara na usafi. Mungu ni mwenye ujuzi wote na asiye na hatia.

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Mungu ni wa namna gani?
JIBU: MUNGU NI ROHO NA MUNGU NI NURU.

+++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

3. **Tena, Mungu ni Pendo.** Kuna mambo mengi katika maisha yanayoweza kutufanya tuwe na tashwishi kuhusu upendo wa Mungu, lakini kila mmoja akielewa sababu gani Mungu alimtuma Mwanawe shaka huondoka.

> **"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."**
> Yohana 3:16

> **"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."**
> Warumi 5:8

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, jina la Mungu ni nini?
JIBU; JINA LA MUNGU NI BWANA.
SWALI: Je, Mungu ni wa namna gani?
JIBU: MUNGU NI ROHO, MUNGU NI NURU, NA MUNGU NI PENDO.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





Kwa hiyo Shetani alifanyika adui wa Mungu na akaliongoza jeshi lipigar na Mungu kama iwezekanavyo. Kwa hiyo, wakati Mungu alipomwumba mtu, Shetani alitaka kumwangusha.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Shetani ni nani?
JIBU: SHETANI NI MKUU WA ROHO WABAYA.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## KAZI WA SHETANI NI NINI?

Maana ya jina lake ni adui. Ni mpinga Mungu na wote wanaomfuata. Kuwajaribu, hudanganya, hutafuta nafasi ya kuwaingiza wengine katika Jehanum. Yeye hufanya kazi yake tu.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Kazi ya Shetani ni nini?
JIBU: KAZI YA SHETANI NI KUMPINGA MUNGU NA WATU WANAOMFUATA.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## MWISHO WA SHETANI NI NINI?

Kudhibiwa milele katika Jehanum utakuwa mwisho wa Shetani na wanaomfuata.

> **"Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti..."**
> Ufunuo 20:10

> **"Kisha atawaambia, na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake."**
> Mathayo 25:41

# DHAMBI NA SHETANI

# 1

**Dibaji**

Kuna maswali mengi huulizwa kuhusu Shetani ambayo hayawezi kujibiwa kwa kuwa Mungu hakutwambia katika Biblia lakini, kuna mambo ya kutosha yaliyofunuliwa kujibu maswali mengi ya kawaida na kutupatia ufahamu wa asili ya adui watu wa kiroho.

**SHETANI NI NANI?**

Biblia humfunua kama mkuu wa roho wabaya, ambao ni wengi. Kuhusu mwanzo wao, hatufahamu mambo mengi. Kutokana na mistari ya maandiko katakatifu, inayofunua jambo kuwahusu, twaamini wakati fulani, lakini chini ya uongozi wa Shetani walimwasi Mungu na wakatupwa mbali naye. Maandiko hutaja juu ya kuanguka kwao:

> **"Na malaika wasioilinda enzi yao mwenyewe, lakini wakayaacha..."**
> **Yuda 6**

> **"Kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu."** **II Petro 2:4**





# MUNGU

# 2

**MARUDIO:**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**SWALI:** Je, jina la Mungu ni nini?
**JIBU;** **JINA LA MUNGU NI BWANA.**
**SWALI:** Je, Mungu ni wa namna gani?
**JIBU:** **MUNGU NI ROHO, MUNGU NI NURU, NA MUNGU NI PENDO.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**MUNGU NI ROHO, MUNGU NI NURU, NA MUNGU NI PENDO, NA PIA:**

**Mungu ni asiye na mpaka wala mwisho.**

**A. Mungu ni wa milele.** Mungu hana mwanzo wala mwisho. Ni Mungu wa milele.

> **"Kabla haijazaliwa milima, wala hujaiumba dunia, na tangu milele hata milele ndiwe Mungu."**
> **Zaburi 90:2**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**SWALI:** Je, Mungu ana mwanzo?
**JIBU:** **HAPANA, MUNGU HANA MWANZO.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

B. Mungu huwa mahali po pote wakati mmoja. Jambo hili halionyeshi anajifanya mwenye na kugawanyika ulimwenguni mwote, lakini huwa kila mahali wakati mmoja tu.

"Ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu. Kwa maana ndani yake yeye, tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu."
Matendo 17:27-28

"Je, mtu ye yote aweza kujificha mahali pa siri, nisimwone?" Asema BWANA. Je, mbingu na nchi hazikujawa nami? Asema BWANA"
Yeremia 23:24

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
SWALI: Je, Mungu yuko wapi?
JIBU: MUNGU YUKO MBINGUNI NA KILA MAHALI.
++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

C. Mungu hujua mambo yote. Anajua yote yaliyopita, na yaliyoko na yatakayokuja. Anajua kila kitu na kila kiumbe.

"Maana hamna neno ulimini mwangu usilolijua kabisa, BWANA."
Zaburi 139:4

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
SWALI: Je, Mungu anajua nini?
JIBU: MUNGU ANAJUA MAMBO YOTE NINAYOYATENDA, NINAYOYASEMA, NA NINAYOYAWAZA.
++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





uvumilivu hata kwa jambo lisilo la haki. Ni kuweza kupokea hata mambo yasiyo ya haki bila kujilipizia, kuweza kufanya shauri na watu wenye kukasirika, bila wewe kukasirika, kuweza kujizuia wakati unapofanyiwa matukano na masingizio.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
SWALI: Je, matunda la Roho Mtakatifu ni nini?
JIBU: UPENDO, FURAHA, NA AMANI, UVUMILIVU, UTU WEMA, NA FADHILI.
++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

3. Pia Roho Mtakatifu hujionyesha kwa mambo yanayohusu mtu peke yake --uaminifu, upole, kujizuia (kiasi). Maana ya uaminifu ni utii kwa watu na kwa Mungu. Upole hauonyeshi kuwa mtu ni mnyonge. Yesu alikuwa mpole, lakini hakuwa mdhaifu. Jambo la mwisho ni kujizuia. Ni lazima kupinge tamaa na mambo maovu ya asili yetu. Wakati mwingine tunashindwa. Uwezo unaoweza humpatia mtu ushindi juu ya mambo haya ni Roho wa Mungu peke yake.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++
SWALI: Je, matunda la Roho Mtakatifu ni nini?
JIBU: UPENDO, FURAHA, AMANI, UVUMILIVU, UTU WEMA, FADHILI, UAMINIFU, UPOLE, NA KUJIZUIA.
SWALI: Je, Roho Mtakatifu ni nani?
JIBU: ROHO MTAKATIFU NI MUNGU.
SWALI: Kazi ya tatu ya Roho Mtakatifu kwa mtu binafsi ni nini?
JIBU:
1. ROHO MTAKATIFU HUTHIBITISHA DHAMBI KWAKE BINAFSI.
2. ROHO MTAKATIFU HUMWONGOZA MWENYE DHAMBI AJUE NJIA YA WOKOVU.
3. ROHO MTAKATIFU HUMSAIDIA MKRISTO KUKUA KIROHO KWA NGUVU NA KUWA KAMA YESU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kazi tatu za Roho Mtakatifu kwa mtu binafsi ni nini?

JIBU: 1. ROHO MTAKATIFU HUTHIBITISHA DHAMBI KWAKE BINAFSI.
2. ROHO MTAKATIFU HUMWONGOZA MWENYE DHAMBI AJUE NJIA YA WOKOVU
3. ROHO MTAKATIFU HUMSAIDIA MKRISTO KUKUA KIROHO KWA NGUVU NA KUWA KAMA YESU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## MAZAO YA ROHO MTAKATIFU NI NINI?

Mazao ya Roho Mtakatifu yameelezwa katika Biblia.

> "Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi, juu ya mambo kama hayo hakuna sheria."
> Wagalatia 5:22-23

1. Matunda ya kwanza ya Roho Mtakatifu ni yale ambayo hujionyesha katika maisha ya kindani -- **Upendo, Furaha, Amani**.

Upendo unaotajwa hapa si fikira za kuvutwa na upendo ili uitwa upendo, ni jambo la kindani, kubwa na la juu, hata kuliko hivyo. Ni asili ya kuongoza jambo la maisha. Jambo lile ambalo linaweza kuwezeshwa na Roho wa Mungu peke yake.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, matunda ya kwanza ya Roho Mtakatifu ni nini?

JIBU: UPENDO, FURAHA, NA AMANI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

2. Na tunda mengine hujionyesha yenyewe katika maisha ya nje -- **Uvumilivu, Utu Wema, Fadhili.** Maana ya uvumilivu ni kutulia kwa





D. **Mungu ana uwezo wote:**

> **"Mara moja amenena Mungu; mara mbili nimeyasikia haya; ya kuwa nguvu zina Mungu."**
> **Zaburi 62:11**

Zaidi ya mara mbili maandiko matakatifu hueleza wazi ya kwamba hakuna jambo lo lote gumu kwa Mungu.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Mungu ana uwezo gani?

JIBU: MUNGU ANA UWEZO WOTE.

SWALI: Jina la Mungu ni nini?

JIBU: JINA LA MUNGU NI BWANA.

SWALI: Je, Mungu ni wa namna gani?

JIBU: MUNGU NI ROHO, MUNGU NI NURU, NA MUNGU NI PENDO. MUNGU NI ASIYE NA MPAKA WALA MWISHO.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## MUNGU MMOJA NDANI YA WATATU

Mafundisho ya Mungu mmoja ndani ya nafsi tatu yanaitwa Utatu. Maana yake ni kwamba Mungu hujifunua kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Ni vigumu kuelewa mafundisho haya kwa haraka, lakini hufundishwa na Biblia. Hatustahili kufikiria ya kwamba jambo si sawa kwa kuwa hatuelewi dhahiri. Mafundisho ya Utatu yanaweza kukosa kueleweka, lakini yanaweza kukubaliwa na kuaminiwa, kwa sababu yamefundishwa wazi katika Biblia.

Twafundisha kuwa Yesu Kristo na Baba ni mmoja.

> "Mimi na Baba tu umoja."
> Yohana 10:30

**"Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, utuonyeshe Baba?"**
**Yohana 14:9**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kuna Mungu mmoja tu?
JIBU: NDIYO, KUNA MUNGU MMOJA TU NDANI YA TATU.
SWALI: Je,Yesu Kristo na Baba ni mmoja?
JIBU: NDIYO, YESU KRISTO NA BABA NI MMOJA.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Twafundisha ya kuwa Yesu Kristo na Roho Mtakatifu ni mmoja. Kama Yesu Kristo alivyofundisha kuhusu Mshauri ambaye ni Roho Mtakatifu aliilinganisha kuwepo kwa Roho Mtakatifu na kuwepo kwake.

**"Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele.. Ndiye Roho wa kweli."**
**Yohana 14:16-17**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Yesu Kristo na Roho Mtakatifu ni mmoja?
JIBU: NDIYO, YESU KRISTO NA ROHO MTAKATIFU NI MMOJA.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Twafundisha tena ya kwamba Mungu na Roho Mtakatifu ni mmoja. Petro alifundisha ya kwamba kumdanganya Roho Mtakatifu ni kumdanganya Mungu.

**"Petro akasema, Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja?.....Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu."**
**Matendo 5:3-4**





kwa dhambi, na hufanya mtu ajue ya kuwa ana hatia mbele ya Mungu.

**"Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha, ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi."**
**Yohana 16:8-9**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kazi ya kwanza ya Roho Mtakatifu kwa mtu binafsi ni nini?
JIBU: KAZI YA KWANZA YA ROHO MTAKATIFU NI KUTHIBITISHA DHAMBI MWAKE BINAFSI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

2. **Na kazi ya pili kwa mtu binafsi: Roho Mtakatifu humwongoza mwenye dhambi ajue njia ya wokovu.** Wakati mtu anapohakikishwa kuhusu dhambi, anaweza kufanya jambo moja kati ya mambo mawili; anaweza kufanya moyo wake kuwa mgumu na amzuie Roho asiingie ndani. Anapoifuata njia hiyo ya nyuma, Roho Mtakatifu huingia ndani ya moyo wako na kufanya kazi ya neema inayoitwa kuzaliwa upya.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, mambo mawili ya kwanza ya kazi ya Roho Mtakatifu kwa mtu binafsi ni nini?
JIBU:
1. KAZI YA KWANZA YA ROHO MTAKATIFU NI KUTHIBITISHA DHAMBI KWAKE BINAFSI.
2. ROHO MTAKATIFU HUMWONGOZA MWENYE DHAMBI AJUE NJIA YA WOKOVU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

3. **Na kazi ya tatu kwa mtu binafsi ni Roho Mtakatifu humsaidia Mkristo kukua kwa nguvu na kuwa kama Yesu.** Kukua huku huja tunaposikiliza kutoka kwa Roho Mtakatifu na kufanya vile yeye hutwambia kufanya.

maisha mapya anapoingia moyoni. Katika Warumi 8:11 ufufuo umetajwa kama kazi ya Roho Mtakatifu.

> " Lakini, ikiwa Roho Wake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu."
> Warumi 8:11

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Roho Mtakatifu ni nani?

JIBU: **ROHO MTAKATIFU NI MUNGU.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Tunaweza kusoma juu ya kuja kwake Roho Mtakatifu katika Matendo 2:1-4.

> "Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka."
> Matendo 2:1-4

## KAZI YA ROHO MTAKATIFU KWA MTU BINAFSI NI NINI?

1. **Roho Mtakatifu huthibitisha dhambi kwake binafsi.** Hufunua kwa mtu jambo la asili ya dhambi, na kuadhibishwa





++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Mungu na Roho Mtakatifu ni mmoja?

JIBU: **NDIYO, MUNGU NA ROHO MTAKATIFU NI MMOJA.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

Kama tunavyofikiria andiko hilo, tunaona kwamba Biblia hutufundisha kwamba Baba na Mwana na Roho Mtakatifu ni umoja. Labda mfano utatusaidia kuelewa vema jinsi umoja unavyoweza kuwa utatu na jinsi utatu unavyoweza kuwa umoja. Fikiria mtu. Inawezekana kwa mtu kuwa bin, mume, na baba wakati moja. Ndiyo ...yeye ni mmoja. Mtu hujitambulisha (au kujulikana) kwa njia tatu. Mungu ni mmoja na kwa hivyo amejitambulisha yeye mwenyewe kama Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, jina la Mungu ni nini?

JIBU: **JINA LA MUNGU NI BWANA.**

SWALI: Je, Mungu ni wa namna gani?

JIBU: **MUNGU NI ROHO, MUNGU NI NURU, NA MUNGU NI PENDO, NA MUNGU NI ASIYE MPAKA WALA MWISHO.**

SWALI: Je, kuna Mungu mmoja tu?

JIBU: **NDIYO, KUNA MUNGU MMOJA TU NDANI YA UTATU.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

# YESU KRISTO

# 1

DIBAJI

Katika fundisho hili tunataka kuona mambo yote muhimu ya Yesu. Tunataka kumwona kama Kristo na Bwana. Tunataka kuanzia na maisha yake ya kimwili na tujifunza kuhusu kuzaliwa kwake, maisha, kifo na ufufuo. Tutamwona kama mtu na tena Mungu.

YESU ALIISHI KABLA YA KUJA ULIMWENGU HUU

Kuwepo kwake Yesu hakukuanzia kama kwa wanadamu wengine kwa kuzaliwa. Aliishi kabla.

1. Kuwa Kristo aliishi kabla ya kuja ulimwengu huu imefundishwa katika Agano Jipya. Mistari michache inaweza kutajwa hapa:

> "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.
> Yohana 1:1-2





# ROHO MTAKATIFU

Dibaji:

Tumejifunza kuhusu Mungu Baba na Mungu Mwana. Sasa tunataka kujifunza nafsi ya tatu; Mungu Roho Mtakatifu. Mara kwa mara mambo mengi ya Roho Mtakatifu hayaeleweki vizuri lakini kwa fundisho hili, tutaona mambo fulani Biblia isemayo kuhusu yeye.

UTU WA ROHO MTAKATIFU

Maandiko huonyesha Roho Mtakatifu kama utu unaoishi na wala si kama mvuto au uwezo unaofanya kazi duniani. Roho Mtakatifu huonyeshwa kama kufanya kazi ya mtu. Hushuhudia, husahihisha makosa, hufariji, hufundisha, huongoza, husumbuka na husaidia. Maneno kama haya hutumika kwa ajili ya mtu. Kama mtu, Roho Mtakatifu huhusika kwa matendo ya watu wengine.

Roho Mtakatifu ni Mungu. Roho Mtakatifu huwako mahali po pote. Ameelezwa kuwa mwenye nguvu katika I Wakorintho 12:11.

> "Lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye." I Wakorintho 12:11

Roho Mtakatifu hufanya kazi ya Mungu. Huthibitisha dhambi. Huleta

2. Ufufuo wa Yesu ulileta hakika ya maisha zaidi ya kaburi. Kwa karne nyingi watu wametafuta dhahiri ya uhakika katika maisha ya milele. Paulo alisema:

> **"Ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele, Na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu; aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili."** II Timotheo 1:9-10

3. Ufufuo wa Kristo ulitoa ahadi na njia ya ufufuo kwa watu wa Kristo .

> **"Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni, kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo, atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu."** Wafilipi 3:20-21

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Yesu Kristo aliishi kabla ya kuja ulimwengu huu?
JIBU: NDIYO, ALIISHI KABLA YA KUJA ULIMWENGUNI.
SWALI: Je, Yesu Kristo ni wa namna gani?
JIBU: YESU KRISTO ALIKUWA MTU KWELI NA ALIKUWA MUNGU KWELI.
SWALI: Je, kwa nini Yesu Kristo alikufa?
JIBU: YESU KRISTO ALIKUFA BADALA YETU.
SWALI: Je, Yesu ni mfu?
JIBU: HAPANA, ALIFUFUKA!

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++





> **"Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye."** Wakolosai 1:16-17

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Yesu Kristo aliishi kabla ya kuja ulimwengu huu?
JIBU: NDIYO, ALIISHI KABLA YA KUJA ULIMWENGUNI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

2. Ukweli ya kwamba Yesu aliishi kabla ya kuja ulimwenguni aliuthibitisha yeye mwenyewe. Zaidi ya mara moja Yesu alieleza kuwepo kwake tangu mwanzo. Kwa Wayahudi ambao hawakuamini alisema:

> **"Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko."** Yohana 8:58

Ibrahimu aliishi karibu na miaka elfu mbili kabla ya Yesu kuzaliwa, lakini kutaja hivyo. Katika maombi ya kuwaombea watu alisema:

> **"Na sasa, Baba,. unitukuze mimi pamoja nawe, kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako."** Yohana 17:5

Yesu Mwana wa Mungu aliyeishi tangu milele, alikuja ulimwenguni na akajivika mwili wa mwanadamu.

> **"Naye Neno (Yesu) alifanyika mwili, akakaa kwetu."** Yohana 1:14

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Yesu Kristo aliishi kabla ya kuja ulimwengu huu?
JIBU: NDIYO, ALIISHI KABLA YA KUJA ULIMWENGUNI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

YESU ALIKUWA MTU KWELI NA MUNGU KWELI

1. Yesu alikuwa mtu kweli. Jina ambalo Yesu aliyejiita akizungumza juu yake mara nyingi lilimkuwa "Mwana wa Mtu." Injili zote husimulia hadithi yake kama mtu. Aliishi kama mtu. Kukua kwa mwili kulikuwa kama kwa wanadamu.

"Naye Yesu akazidi kuendelea kwa hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu."
Luka 2:52

2. Yesu alikuwa Mungu kweli. Yesu hakuwa mwana wa Mtu tu, bali alikuwa Mwana wa Mungu pia. Yeye mwenyewe alisema hivyo.

"Aliyeiona mimi amemwona Baba."
Yohana 14:9
"Mimi na Baba tu umoja."
Yohana 10:30

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Yesu Kristo ni wa namna gani?
JIBU: YESU KRISTO ALIKUWA MTU KWELI NA ALIKUWA MUNGU KWELI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

YESU NI MTAKATIFU

1. Yesu ni Mtakatifu kwa sababu kuzaliwa kwake kulikuwa kutakatifu . Hakujawahi kutokea kuzaliwa kwa ajabu kama kule kuzaliwa kwa mtoto katika Bethlehemu; Mathayo husema:

"Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu."
Mathayo 1:18

Luka hueleza hadithi hii kama Mathayo hata kuweka mkazo zaidi.





"Kama ni hivyo, ingalimpasa kuteswa mara nyingi tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu; lakini sasa, mara moja tu, katika utimilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake...Kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi."
Waebrania 9:26, 28

KUFUFUKA KWA YESU

Kristo alikufa msalabani na akazikwa katika kaburi la Yusufu. Lakini leo si mfu! Siku ya tatu alifufuka kutoka kaburini na anaishi milele.

"Tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena."
Warumi 6:9

1. Kufufuka kwa Yesu kulimaliza kazi ya msalaba. Kristo mfu hangalikuwa Mwokozi. Paulo alisema:

"Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu."
I Wakorintho 15:17

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Yesu ni mfu?
JIBU: HAPANA, ALIFUFUKA!

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

1. Kifo cha Yesu Kristo kilikuwa cha kuonyesha upendo wa Mungu. Yesu hakwenda msalabani kwa sababu hangeweza kujisaidia kutoka kwa adui zake.

"Kwa sababu nautoa uhai wangu ili niutwae tena, hakuna aniondoleaye, bali mimi nautoa mwenyewe."
Yohana 10:17-18

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Yesu Kristo aliwaonyesha watu pendo lake?
JIBU: NDIYO, YESU KRISTO ALIWAONYESHA WATU PENDO LAKE.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

2. Yesu Kristo alikufa badala yetu.

"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye."
2 Wakrointho 5:21

"Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu." Wagalatia 3:13

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kwa nini Yesu Kristo alikufa?
JIBU: YESU KRISTO ALIKUFA BADALA YETU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

3. Yesu alikufa mara moja kwa watu wote. Hatutakuwa na Mwokozi mwingine kwa kuwa ulimwengu hautahitaji mwingine.





**"Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu."** **Luka 1:35**

Wanaokataa Ubikira wa kuzaliwa kwa Yesu huukataa ukweli wa Neno la Mungu.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kwa nini tunaweza kujua Yesu ni mtakatifu?
JIBU: YESU NI MTAKATIFU KWA SABABU KUZALIWA KWAKE KULIKUWA KUTAKATIFU.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

2. Twajua ya kuwa Yesu alikuwa Mtakatifu kwa sababu ya maisha **aliyoishi**. Yesu aliishi maisha ya haki. Mwandishi wa Waraka wa Waebrania alisema kuhusu yeye hivi:

**"Bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi."**
**Waebrania 4:15**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kwa nini tunaweza kujua Yesu ni mtakatifu?
JIBU: YESU NI MTAKATIFU KWA SABABU KUZALIWA KWAKE KULIKUWA KUTAKATIFU NA KWA SABABU YA MAISHA ALIYOISHI.
SWALI: Je, Yesu Kristo aliishi kabla ya kuja ulimwengu huu?
JIBU: NDIYO, ALIISHI KABLA YA KUJA ULIMWENGUNI.
SWALI: Yesu Kristo ni wa namna gani?
JIBU: YESU KRISTO ALIKUWA MTU KWELI NA ALIKUWA MUNGU KWELI.

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

# YESU KRISTO

# 2

MARUDIO:

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, Yesu Kristo aliishi kabla ya kuja ulimwengu huu?
JIBU: **NDIYO, ALIISHI KABLA YA KUJA ULIMWENGUNI.**
SWALI: Yesu Kristo ni wa namna gani?
JIBU: **YESU KRISTO ALIKUWA MTU KWELI NA ALIKUWA MUNGU KWELI.**
SWALI: Je, kwa nini tunaweza kujua Yesu ni mtakatifu?
JIBU: **YESU NI MTAKATIFU KWA SABABU KUZALIWA KWAKE KULIKUWA KUTAKATIFU NA KWA SABABU YA MAISHA ALIYOISHI.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

YESU NI MTAKATIFU KWA SABABU KUZALIWA KWAKE KULIKUWA KUTAKATIFU, KWA SABABU YA MAISHA ALIYOISHI:

**Twajua ya kuwa Yesu alikuwa Mtakatifu kwa mambo aliyofundisha.** Wakati watu walipotumwa kutoka Yerusalemu wakamshike na kumpeleka kwa mahakimu, walirudi bila yeye. Walipoulizwa kuhusu kushindwa kwao, walijibu:





> **"Hajanena kamwe mtu ye yote kama huyu anavyonena."** Yohana 7:46

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, sababu tatu twajua ya kuwa Yesu alikuwa mtakatifu ni nini?
JIBU: **NI KWA SABABU KWA MAMBO ALIYOFUNDISHA.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

**Twajua ya kuwa Yesu alikuwa Mtakatifu kwa sababu ya utukufu wa ufufuo wake.** Paulo alithibitisha kuwa, ufufuo wa Yesu alikuwa hakikisho la kweli la Uungu wake:

> **"Yaani, habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya Mwili, na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu."** Warumi 1:3-4

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

SWALI: Je, kwa nini tunaweza kujua Yesu ni mtakatifu?
JIBU: **TUNAJUA YESU NI MTAKATIFU KWA SABABU KUZALIWA KWAKE, MAISHA ALIYOISHI, MAMBO ALIYOFUNDISHA, NA UTUKUFU WA UFUFUO WAKE.**

++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++++

## KIFO CHA KRISTO

Kuangikwa msalabani kwa Yesu ilikuwa hatia ya nyakati zote, ulikuwa ukuu wa kuthibitisha upendo wa Mungu.

> **"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."** Warumi 5:8